

Kufunga Suction Hose

Lini tunafunga suction hose na kwa nini?

- Tunafunga suction hose kama amri ikiwa „Chanzo cha maji ni kisima/bahari“
- Tunahitaji suction hose kunyonya maji kupeleka kwenye tenki ya gari kwa hivyo tunaweza kutumia maji mengi

Tunahitaji nini?

- suction hose, chujio, kikapu cha kuzuia, funguo mbili, kamba ya koki, kamba ya kuvuta
- Kundi B, (Kundi C), Pump Operator

Kubeba suction hose

- Watu wawili wanabeba suction hose mbili (mmoja mbele, mmoja nyuma)
- Mtu mmoja anabeba suction hose moja (mkono moja unashika karibu na coppling chini, mkono moja unashika juu) → Tunabeba suction hose juu tu, kwa hivyo hatuwezi kuumia mtu mwingine

Kufunga/kufungua coppling

- Tunashika ufunguo na mkono wa kulia tu na tunasogeza ufunguo chini tu
- Watu wawili wanakaa juu ya suction hose na wanashika coppling binafsi
- Tunafunga kwanza na mikono, alafu na funguo (kushoto = kufungua; kulia = kufunga)
- Kwa kufungua: Tunasogeza coppling kulia tena, lakini kila mtu anasogeza coppling ya mtu mwingine

Vipi tunafunga suction hose?

- Kiongozi wa Kundi B anatoa amri suction hose ngapi. Kwa mfano “Suction hose 3!”
- Pump Operator anachukua vifaa na anachoweka mbele. Anaanza na chujio na funguo
- Kundi B na C wanaweka suction hose kwa mstali moja
- Kundi B wanafunga kila coppling, lakini wanaanza kwenye chujio. Wanakaa juu ya suction hose na wanaweka funguo kulia ya suction hose. Wanafunga coppling kidogo na mikono (geuza coppling kulia) alafu wanafunga kabisa na funguo. Kila mara tunashika funguo na mkono wa kulia tu!
- Kundi C wanakaa nyuma ya Kundi B. Wanasaidia kushika na kusogeza suction hose kwa hivyo Kundi B wanaweza kufunga coppling. Kundi B wanatoa amri “chini”, “juu”, “kushoto”, “kulia”
- Kiongozi wa Kundi B anatoa amri “Shikeni suction hose!”
- Watu watatu wanashika suction hose karibu na tumbo lao. Wote wanakaa upande mmoja mbali ya maji. Kiongozi wa Kundi B anafunga kamba ya kuvuta kwenye chujio na suction hose na kitanzi cha macho kawaida pamoja na kitanzi chenye usalama zaidi au kitanzi cha kunyanyua mbao. Alafu anafunga kitanzi nusu kwa kila coppling.
- Kiongozi wa Kundi B anafunga kamba ya koki kwenye koki ya chujio, akasema “Hatari, Kamba!” na anarusha kamba mpaka mwisho ya suction hose
- Alafu anafunga kikapu cha kuzuia - Ni lazima kwamba koki inaweza kusogea bado!
- Akimaliza anatoa amri “Suction hose kwenye gari!”
- Pump Operator anafunga suction hose kwenye pump, alafu anatoa amri “Tayari!”
- Kiongozi wa Kundi B anatoa amri “Suction Hose kwenye kisima/bahari!”
- Pump Operator anafunga kamba ya kuvuta na kitanzi cha macho kawaida kwenye nafasi fulani